

## 2. Wajiitao Watumishi

### wa Mungu

**K**una watu wengi wanaojiita Wachungaji, au watumishi wa Mungu, lakini sio, bali ni Mafisi. Katika eneo hili la watumishi wa Mungu kuna tatizo kubwa sana la kupatikana watumishi wa Mungu ambao kwa asilimia kubwa sio wa kweli, bali ni waovu na wamekusudia kufanya uovu mkubwa katika Kanisa na kwa waumini wale wanaowaendea.

*Mathayo 7:15.19 Jihadharini na **manabii wa uongo, watu wanaowajia wamevaa mavazi ya kondoo, walakini kwa ndani ni mbwa-mwitu wakali.** Mtawatambua kwa matunda yao. Je! Watu huchuma zabibu katika miiba, au tini katika mibaruti? Vivyo hivyo kila mti mwema huzaa matunda mazuri; na mti mwovu huzaa matunda mabaya. Mti mwema hauwezi kuzaa matunda mabaya, wala mti mwovu kuzaa matunda mazuri. Kila mti usiozaa tunda zuri hukatwa ukatupwa motoni.*

Yesu alitangulia kusema kuwa, kuna manabii wa uongo au watumishi wa uongo, ambao watu wanaowajia hali wamevaa mavazi ya kondoo lakini kwa ndani ni mbwa mwitu wakali. Ni kwamba, hawa ni watumishi wanaojiingiza huku wakijua kuwa wao sio watumishi wa Mungu, lakini wameamua kwa makusudi kuingia katika huduma kwa malengo ya kuchukua wanavyovitaka ndani ya Kanisa la Mungu. Kubwa zaidi ni kuwatumia vibaya waumini waliomo Kanisani. Masharti yote yanayohitajika wapo tayari kuyafuata hata kama kwa unafiki,

wakiambiwa waokoke watajifanya wapo tayari kuokoka, wakiambiwa waende kusoma, wapo tayari kwenda kusoma, lakini lengo lao baada ya hayo wapate uwanja wa kuwatumia kondoo kwa masilahi yao binafsi. Hayo Mafisi yapo yenye elimu kubwa ya dini, yapo yenye kujua vizuri maandiko, yapo yenye kujifanya yapo kiroho sana.

Siku za karibu serikali nyingi za duniani, hata hapa Afrika Mashariki, walikumbwa na fikira za kuwalazimisha watumishi wa Mungu wahakikishe wanasoma vyuo vya Thiolojia ili kuongeza elimu zao. Lakini zipo serikali zilizozuia kabisa watumishi wasio na elimu ya chuo cha Biblia wasihuduma bali waache huduma hadi watakapotimiza masharti hayo. Serikali hizo ziliamini kuwa, kwa kutokuwa na elimu ya chuo cha Biblia ndio chanzo cha vitendo vya kihuni Makanisani, lakini kihali-sia kuna wenye elimu kubwa tu ya Thiolojia lakini nao wanafanya vitendo vya kihuni.

Mafisi wanafanya makosa makusudi na sio kwa bahati mbaya, au kwa sababu hawajui kuwa wanalolifanya kuwa ni kosa au ni dhambi, bali wanafanya huku wakijua kila kitu kuwa sio sahihi, ila kwa kuwa wao ni Mafisi na hawanakusudi la kumuogopa Mungu, hivyo hufanya makusudi.

Ninachosema, Mafisi kila mahali wanaweza kufika, kila kitu wanaweza kufanya. Kwa ujumla haya mambo ya uhalifu kupitia imani hayawezi kuzuilika kirahisi, kwani hayo yalitabiriwa kuwa yatakuwepo. Hivyo kuweka masharti makali ya kuwatumia watumishi sahihi, sio jawabu la kuwazuia Mafisi.